**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI-VETA DODOMA KANDA YA KATI. UJENZI WA CHUO CHA VETA CHA WILAYA YA IKUNGI**

**(IKUNGI DVTC)**

---

______ KOTESHENI TAREHE YA KUJAZA: 12/03/ KWA;

STEPHANO WILLIAM NGONYA. ANUANI: 485 BABATI

**YAH: KUFANYA KAZI ZOTE ZA UMEME ( AWAMU YA KWANZA,AWAMU YA PILI NA AWAMU YA TATU ) " FIRST FIX ,SECOND FIX AND THIRD FIX"**

Tafadhali jaza bei shindanifu kwa ajili ya kazi tajwa hapo chini katika majengo ya chuo cha ufundi stadi (VETA) Ikungi, Bei zako zitashindanishwa na Mafundi wengine na kuangaliwa uhalisia wake, jaza bei kwa majengo yote,

| No. | JENGO | MAELEZO YA KAZI | GHARAMA ZA FUNDI |
|---|---|---|---|
| 01 | UTAWALA | Mifumo yote ya umeme | 1,600,000/= |
| 02 | MADARASA | Mifumo yote ya umeme | 1,400,000/= |
| 03 | STOO | Mifumo yote ya umeme | 500,000/= |
| 04 | JIKO NA BWALO LA CHAKULA | Mifumo yote ya umeme | 1,400,000/= |
| 05 | HOSTELYA WAVULANA | Mifumo yote ya umeme | 1,600,000/= |
| 06 | HOSTEL YA WASICHANA | Mifumo yote ya umeme | 1,600,000/= |
| 07 | NYUMBA YA MKUU WA CHUO | Mifumo yote ya umeme | 1,000,000/= |
| 08 | NYUMBA YA WATUMISHI | Mifumo yote ya umeme | 1,000,000/= |
| 09 | KARAKANA YA DSCT | Mifumo yote ya umeme | 1,500,000/= |
| 10 | KARAKANA YA COMPUTA &SECR | Mifumo yote ya umeme | 1,500,000/= |
| 11 | KARAKANA YA UASHI NA UMEME | Mifumo yote ya umeme | 1,500,000/= |
| 12 | KARAKANA YA MAGARI NA UCHOMELEAJI | Mifumo yote ya umeme | 1,600,000/= |
| 13 | CHOO CHA WASICHANA | Mifumo yote ya umeme | 100,000/= |
| 14 | CHOO CHA STAFU | Mifumo yote ya umeme | 100,000/= |
| 15 | CHOO CHA WAVULANA | Mifumo yote ya umeme | 100,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 16 | NYUMBA YA KUFUA UMEME | Mifumo yote ya umeme | 200,000/= |
| 17 | NYUMBA YA MLINZI | Mifumo yote ya umeme | 100,000/= |
| | | **JUMLA YA GHARAMA** | 16,200,000/= |
| | | | |

Kwa masharti yaliyoainishwa hapa, Kotesheni hii ikishajazwa irudishwe ofisi ya muda ya Wasimamizi wa kazi (Iliyopo eneo la kazi) au ofisi za Kanda iliyopo Dodoma kabla ya tarehe 08/04/2022

1. Fundi hakikisha umejaza bei za kazi kwa kila jengo. 2. Fomu haitapokelewa endapo haija kamilika kujazwa. 3. Mawasiliano yote kuhusu vifaa vya kazi yatafanywa kupitia ofisi ya Wasimamizi wa kazi 4. Migogoro kati ya Fundi Mkuu na wasaidizi wake au vibarua yatatatuliwa na Wasimamizi wa kazi (Ofisi ya Mhandisi Msimamizi wa kazi) 5. Fundi hakikisha umesaini kila ukurasa wa kotesheni yako

John Thomas

..............................

Saini ya Mhandisi

**Tarehe:** 12/8/2022

..............................

Saini ya fundi

**Tarehe:** 12/3/2022

11. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri *(kutokana na fedha au vifaa)*, Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.

12. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi mkuu au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi mkuu au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.

13. Mkataba utavunjwa endapo fundi mkuu atashindwa kuajiri mafundi wasaidizi kulingana na ukubwa wa kazi,kama itakavyoelekezwa na washauri,ama kamati.

14. Hakutakuwa na ongezeko la gharama zitakazotokana na ongezeko la muda wa mkataba.

**MWAJIRI:**

Saini: ..............................

Jina: John R. Ruwanja

Cheo: RD

Tarehe: 12/3/2022

**FUNDI/~~KIBARUA~~**

Saini: ..............................

Jina: STEPHANO WILLIAM NGONYA

Cheo: TECHNICIAN

Tarehe: 12/03/2022

**SHAHIDI WA MWAJIRI**

Saini: ..............................

Jina: JoHN THOMAS

Cheo: MSIMAMIZI WA MRADI

Tarehe: 12/03/2022

**SHAHIDI WA FUNDI /KIBARUA**

Saini: ..............................

Jina: WILMARK NKINI

Cheo: FUNDI UMEME

Tarehe: 12/03/2022

B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kama mcganga,kokoto,nondo,cement,mbao,marine n.k kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Fundi mkuu atalazimika kuja na vifaa vyake vya kifundi na usalama eneo lake la kazi kama; refrector,panga,sururu,chepe,ndoo,jembe,safety boot,kofia ngumu n.k
3. Fundi mkuu atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
4. Fundi mkuu asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
5. Fundi mkuu atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
6. Fundi mkuu kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
7. Fundi mkuu atahusika na vitendo *(kama wizi, uharibifu wa mali za chuo)* vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
8. Fundi mkuu kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
9. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika *(Retention Money)* na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.
10. Ucheleweshaji wa Kazi:

    - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.